



Kongamano la  
Kiswahili  
Bayreuth



UNIVERSITÄT  
BAYREUTH

## Kongamano la Ishirini na Nane la Kiswahili Bayreuth

Iwalewahaus, 30 Mei hadi 2 Juni 2015

21 Aprili 2015

Waalikwa Wapendwa – Mabibi na Mabwana,

Kwa mara nyingine tunawashukuruni sana kwa kuuitika mwito wetu. Kwa furaha tumepokea mihtasari na makala yenu. Kukutana nanyi nyote hapa kwetu itakuwa furaha hata zaidi. Karibuni sana!

Katika barua hii ya pili tunawatumia pia ratiba ya kongamano la mwaka huu, kama ilivyo kwa wakati huu. Kongamano la mwaka huu litafanyika *Iwalewahaus* – jumba jipya la Taasisi ya Sanaa za Afrika ya Chuo Kikuu cha Bayreuth. *Iwalewahaus* itafunguliwa tena rasmi siku moja kabla ya kongamano letu – kwa hiyo kongamano hili letu la mwaka huu ni mkutano wa kwanza kabisa katika jumba hili jipya la *Iwalewahaus*. Anwani ni: Iwalewahaus, Wölfelstr. 2, 95444 Bayreuth. Kongamano litaanza **Jumapili tarehe 31 Mei**, saa mbili na nusu asubuhi. Kujisajili kutagarimu Euro 15 kwa wasio wanafunzi / Euro 10 kwa wanafunzi wageni.

Siku moja kabla ya Kongamano, yaani **Jumamosi tarehe 30 Mei**, hatutakutana kwa chakula cha jioni kama ilivyo kawaida yetu. Hata hivyo, kwa kutegemea uwezekano wenu, mnapendekezewa kuhudhuria matukio mawili. La kwanza, mnaalikwa kwenda *Iwalewahaus* ambayo itakuwa na sherehe za kufunguliwa rasmi baada ya kuhama na kujengwa kwa mwaka mmoja u nusu. Jioni hii mnakaribishwa kutazama (kufunguliwa kwa) maonyesho ya sanaa ya yanayoitwa *Mashup*. Shughuli hii itaanza rasmi saa moja jioni, halafu saa nne ni sherehe. Kwa habari zaidi tafadhali tazama matangazo tunayowaambatishia. Pili, kabla ya kwenda *Iwalewahaus*, mnaweza kwenda kutumbuizwa kwa nyimbo za *Kwaya ya Kiswahili ya Bayreuth* kuanzia saa kumi na moja alasiri katika ukumbi wa *Audimax wa Chuo Kikuu cha Bayreuth* (*Audimax Theaterraum*) uliopo kwenye *campus* ya chuo. *Kwaya ya Kiswahili ya Bayreuth* imetimiza miaka kumi tangu kuanzishwa na siku hii wanakwaya watafanya tamasha za kusherehekea hili. *Kwaya* hii ilianzishwa na inahudhuriwa na wanafunzi (pamoja na waliohitimu uanafunzi) wa masomo mbali mbali na waliokuwa na haja ya kuimba kwa Kiswahili. Habari za ziada zinazopatikana kwenye ambatisho tunalowatumieni.

Bali na hayo kongamano letu lina mambo ya ziada: **Jumapili jioni**, Sam Hopkins, msanii Mkenya aliye mtayarishi wa maonyesho ya *Mashup* pamoja na naibu mkurugenzi wa *Iwalewahaus* Bi. Nadine Siegert, watatuonyesha na kutueleza kuhusu maonyesho hayo.

**Siku ya Jamutatu jioni**, tutawakaribisha washiriki kwa chakula na kinywaji na baadaye tutakuwa na kikao cha fasihi. Karibu nasi kutakuwa na kongamano la *African Literature Association* (ALA), litakalofanyika Bayreuth baada ya Kongamano la Kiswahili. Kwa kuunga udugu na ALA na kwa kuwa watu kadha wanaojishughulisha na kumtafsiri Kezilahabi watakuwa nasi, watafsiri watatusomea tafsiri zao za ushairi na riwaya za Euphrase Kezilahabi.

Ukikitaji habari zaidi kuhusu Kongamano la ALA litakalofanyika kuanzia tarehe 3 Juni 2015, tazama <http://www.ala2015.com/#/home/>

Kwa walioomba kusaidiwa kupata malazi hasa nyumbani kwa wanafunzi wetu wakati wa kongamano, tutawaandikia muda si mrefu. Kama kuna wanafunzi wengine watakaopenda kuja na wanahitaji usaidizi wa malazi au kama una maswali yoyote ya ziada, usisite kuwasiliana nasi. Anwani ni: [swahili@uni-bayreuth.de](mailto:swahili@uni-bayreuth.de)

Karibuni sana!

Salamu nyingi,

Ni sisi wenyeji wenu,

Clarissa Vierke, Roberto Gaudioso na Fred Bosire

Universität Bayreuth

Literaturen in afrikanischen Sprachen (GW I, Raum: 1.10)

95440 Bayreuth

Telefon: + 49 921 55-3550

Fax: + 49 921 55-3641

[swahili@uni-bayreuth.de](mailto:swahili@uni-bayreuth.de)

[http://www.afrikanistik.uni-bayreuth.de/de/colloq/swahili\\_colloq/index.html](http://www.afrikanistik.uni-bayreuth.de/de/colloq/swahili_colloq/index.html)

**DFG**